# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUBADILISHA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana leo katika Baraza lako Tukufu. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie wepesi na ufasaha katika kuwasilisha hotuba hii pamoja na kutupa usikivu na uelewa wa kina ili tuweze kujadili kwa umakini na hatimaye kuupitisha Mswada huu wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada huu wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Hotuba hii ni matakwa ya Kanuni ya 91(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2024 ambayo inamtaka Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Mswada kutoa taarifa kuhusu maoni ya Kamati juu ya Mswada huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa hotuba hii na kuweza kuiwasilisha mbele ya Baraza lako kumetokana na michango na mashirikiano makubwa niliyopata kutoka kwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bajeti. Vilevile, naishukuru kwa dhati Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa uratibu na usaidizi wao katika kufanikisha kazi za Kamati na maandalizi ya hotuba hii. Kwa kuthamini na kutambua mchango wao mkubwa kwa Kamati, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Said Khamis | Makamo Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Farida Amour Mohammed | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Ali Salim | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Ali Hassan | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu Kamati |
| 9. | Ndg. Maryam Mohammed Othman | Katibu Kamati |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu Kamati |
| 11. | Ndg Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu Kamati |
| 12. | Ndg. Said Bakar Hamad | Msaidizi wa Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa watendaji wa Idara ya Ushauri wa Kisheria pamoja na Kitengo cha Bajeti cha Baraza kwa kuipatia Kamati ushauri wa kitaalamu katika masuala ya sheria na kodi, jambo ambalo limeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Baraza lako kwamba, matakwa yote ya kikanuni ambayo yanaelekeza Miswada ya Sheria kupitishwa katika ngazi ya Kamati kabla ya kuja kuwasilishwa Barazani yametekelezwa. Kamati ya Bajeti ilipitia kwa kina Mswada huu na pia ilipata fursa ya kukutana na kujadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuujadili kwa kina na hatimae kuupitisha.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukrani hizo, naomba sasa kuanza kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2026.

## UCHAMBUZI WA MSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imepanga kuchukua hatua mbalimbali zinazohusu marekebisho ya Sheria pamoja na hatua za kuimarisha utawala na usimamizi wa kodi. Mswada huu wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2026 unaelezea hatua zinazohusu marekebisho ya sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nam. 7 ya 2009 ambayo inalenga kuimarisha

usimamizi wa kodi, kuimarisha usajili na uthibitisho wa walipakodi, na kuongeza uwazi katika uoneshaji wa nambari au vyeti vya usajili wa kodi. Aidha, marekebisho hayo yanaweka masharti mapya ya adhabu, kuruhusu kuongezewa muda wa kulipa kodi kwa sababu za msingi, na kuimarisha usimamizi wa watoa huduma za malipo ya kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na marekebisho yaliyopendekezwa katika sheria hii, pamoja na kupendekeza marekebisho yake katika Kifungu cha 4 kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake. Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya kidijitali ya kodi, kuongeza elimu kwa walipakodi, na kuhakikisha uwazi na urahisi katika utekelezaji wa sheria hii ili kuendana na mazingira halisi ya biashara Zanzibar. Vilevile, adhabu ziwe za uwiano na zisizoathiri wafanyabiashara wadogo, huku ushirikiano kati ya ZRA na TRA – Zanzibar na watoa huduma za malipo ya kielektroniki kuimarishwa ili kuongeza mapato na kuimarisha ulipaji kodi kwa hiari.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine inayorekebishwa ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998, ambapo marekebisho hayo yanalenga kuimarisha ukusanyaji wa kodi katika sekta ya utalii. Aidha, inapendekezwa kwamba mlipakodi aliyesajiliwa kupitia ZIPA ambaye anatoa huduma za hoteli au utalii hataruhusiwa kupunguza kodi katika ununuzi ya vifaa vya ujenzi, ukarabati au uimarishaji wa mali za kudumu kama majengo, samani na vifaa vingine vinavyotumika katika huduma hizo ili kuimarisha usawa na ufanisi katika mfumo wa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na marekebisho ya Sheria hii sambamba na kuishauri Serikali kuhakikisha utekelezaji wa marekebisho hayo unafanyika kwa kuzingatia mazingira halisi ya sekta ya utalii, ili kuepuka kuathiri uwekezaji. Vilevile, kuwepo na elimu ya kutosha kwa wawekezaji na walipakodi ili kuelewa masharti mapya ya VAT na kuhakikisha utii wa kodi unaimarika bila kuleta usumbufu katika shughuli za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ushuru wa Stempu, Nam. 7 ya 2017 nayo inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kupunguza kiwango cha ushuru wa stempu kwa asilimia 25 kwa gari za biashara pamoja na kuweka utaratibu wa ulipaji wa ushuru huo wakati wa upasishaji wa gari. Hatua hii imelenga kuimarisha utii katika ulipaji kodi na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono marekebisho hayo na kupendekeza marekebisho yake katika Kifungu cha 13 kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake.

Sambamba na hayo, Kamati inaishauri kuwa kabla ya utekelezaji wa marekebisho hayo, Serikali itoe elimu ya kutosha kwa walipakodi wanaojihusisha na biashara ya usafirishaji wa gari ili kuwawezesha kufahamu ipasavyo masharti mapya ya kodi. Hatua hiyo itasaidia kupunguza malalamiko na mkanganyiko unaoweza kujitokeza kutokana na ulipaji wa kodi na tozo nyingine kwa wakati mmoja wakati wa usajili au upasishaji wa gari za biashara, na hivyo kuimarisha utii katika ulipaji wa kodi kwa hiari na ufanisi katika utekelezaji wa sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine inayorekebishwa ni Sheria ya Ushuru wa Hoteli, Nam. 1 ya 1995, ambapo marekebisho hayo yanalenga kuleta mtiririko mzuri wa vifungu ili kuimarisha uwazi, mpangilio na urahisi wa utekelezaji wa sheria hiyo. Kamati inaafikiana na marekebisho hayo na inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, kwani yatasaidia kurahisisha mazingira ya uwekezaji katika hoteli Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mswada huu, Sheria nyengine inayorekebishwa ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017, ambapo marekebisho hayo yanalenga kurahisisha usimamizi wa ushuru kwa bidhaa zinazoingia Zanzibar kutoka Tanzania Bara, kwa kuweka utaratibu wa kufidia ulipaji wa tofauti ya ushuru kulingana na viwango vinavyotumika, ili kuimarisha uwiano wa kodi na kurahisisha biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kwa kuwa yatasaidia kuimarisha biashara na kuzuia mianya ya upotevu wa mapato. Aidha, Kamati inapendekeza marekebisho yake katika Kifungu cha 18 kwa lengo la kusomeka vizuri na kuimarisha utekelezaji wake. Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwepo kwa utaratibu madhubuti wa kukadiria tofauti ya ushuru ili kuepusha mkanganyiko kwa wafanyabiashara na kulinda mazingira ya biashara Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mswada huu, Serikali pia inalenga kurekebisha Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 8 ya 2006, ambapo marekebisho hayo yanahusu kupunguza kiwango cha makato ya michango kutoka asilimia nne hadi asilimia tatu, kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa sekta binafsi na hivyo kuziwezesha kuimarisha ubora wa huduma wanazotoa kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaafiki marekebisho hayo kwa kuwa yatapunguza gharama za uendeshaji na hatimae kuimarisha uwezo wa sekta binafsi kuwekeza zaidi katika rasilimali watu, vifaa na mafunzo, jambo litakalosaidia kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma za elimu na kuchangia maendeleo ya jamii kwa ujumla. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kupunguza tozo hii SDL hadi kufikia asilimia 1 au

kuiondosha kabisa, kwa kuzingatia kuwa sekta binafsi inachangia kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa huduma kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine inayorekebishwa ni Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), Nam. 9 ya 2015, ambapo marekebisho hayo yanalenga kupanua wigo wa msamaha wa kodi kwa kuhusisha usambazaji wa vifaa saidizi, vifaa tiba na vifaa vyengine maalumu kwa matumizi ya watu wenye ulemavu, kwa lengo la kuimarisha ujumuishi na kupunguza gharama kwa makundi yenye mahitaji maalum.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kwa kuwa yataimarisha ustawi wa watu wenye ulemavu kupitia upatikanaji rahisi wa vifaa saidizi na vya tiba. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa uwazi na uadilifu ili kuzuia matumizi mabaya ya msamaha huo, pamoja na kuimarisha upatikanaji wa vifaa hivyo kwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine Sheria inayorekebishwa katika Mswada huu ni Sheria ya Uwekezaji Zanzibar, Nam. 10 ya 2023, ambapo inakusudiwa kuimarisha uwajibikaji wa wawekezaji katika matumizi ya misamaha ya kodi kwa kuweka adhabu kwa watakaothibitika kuitumia isivyo sahihi, ikiwemo ulipaji wa kodi husika pamoja na faini, na kuondoa uwezekano wa kupewa msamaha mwingine wa kodi, ili kulinda mapato ya Serikali na kuimarisha nidhamu ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaafiki marekebisho hayo kwa kuwa yataimarisha uwajibikaji wa wawekezaji na kulinda mapato ya Serikali dhidi ya matumizi yasiyo sahihi ya misamaha ya kodi. Aidha, Kamati inapendekeza marekebisho yake katika Kifungu cha 24 kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake. Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha uwepo wa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na ukaguzi ili kubaini mapema matumizi yasiyo sahihi ya misamaha hiyo, pamoja na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa haki na uwazi ili kutoathiri mazingira ya uwekezaji Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya mwisho inayorekebishwa katika Mswada huu ni Sheria ya Ajira, Nam. 11 ya 2005, ambapo lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika mahusiano ya kazi kwa kuwataka waajiri kutoa taarifa muhimu za ajira kama mikataba, idadi ya wafanyakazi na masharti ya utumishi, na kuweka adhabu kwa watakaoshindwa kutekeleza masharti hayo ili kulinda haki za wafanyakazi na kuimarisha usimamizi wa ajira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kwa kuwa yataimarisha uwazi, uwajibikaji na ulinzi wa haki za wafanyakazi katika sekta ya ajira. Aidha, Kamati inapendekeza marekebisho yake katika Kifungu cha 26 kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake. Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii unazingatia ushirikiano wa karibu kati ya waajiri na mamlaka husika ili kuepusha kutofautiana, pamoja na kutoa elimu ya kutosha kwa waajiri kuhusu masharti mapya ili kuhakikisha utii wa sheria bila kuathiri mazingira ya biashara na ajira.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kupata ufafanuzi wa kina wa marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Bajeti, nawaomba Wajumbe wako waupitie Waraka wa Kamati wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu ambao wamepatiwa.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kuuchangia na hatimae kuupitisha Mswada huu ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kuweka mfumo bora wa kodi na wenye kutabirika, kushajihisha ulipaji wa kodi kwa hiari, kuongeza mapato ya Serikali na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee, Kamati inapenda kutoa shukrani za dhati kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Dkt. Juma Malik Akil, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Hamad Omar Bakar, pamoja na watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla. Kwa pamoja walishiriki katika kikao cha Kamati na kutoa ufafanuzi wa kina pale ulipohitajika. Ushirikiano wao umechangia kwa kiasi kikubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimae kuweza kuwasilisha hotuba hii ya maoni yake mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa utulivu na kwa umakini mkubwa katika kipindi chote nilipokuwa nawasilisha Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti,

naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………..

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**